BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR 2016 - 2020

1.	**Mhe.**	**Zubeir Ali Maulid**	**-**	**SPIKA**
2.	**Mhe.**	**Mgeni Hassan Juma**	**-**	**Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake**
3.	**Mhe.**	**Shehe Hamad Mattar**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni**
4.	**Mhe.**	**Mwanaasha Khamis Juma**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani**
5.	**Mhe.**	**Balozi Seif Ali Iddi**	**-**	**MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda**
6.	**Mhe.**	**Issa Haji Ussi Gavu**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka**
7.	**Mhe.**	**Haji Omar Kheri**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu**
8.	**Mhe.**	**Haroun Ali Suleiman**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi**
9.	**Mhe.**	**Mohammed Aboud Mohammed**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Uteuzi wa Rais**
10.	**Mhe.**	**Dkt. Khalid Salum Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge**
11.	**Mhe.**	**Mahmoud Thabit Kombo**	**-**	**MBM/Waziri wa Habari, Utalii, na Mambo ya Kale/Jimbo la Kiembesamaki**
12.	**Mhe.**	**Riziki Pembe Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake**
13.	**Mhe.**	**Balozi Amina Salum Ali**	**-**	**MBM/Waziri wa Biashara, na Viwanda / Uteuzi wa Rais**
14.	**Mhe.**	**Balozi Ali Abeid Karume**	**-**	**MBM/Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Uteuzi wa Rais**
15.	**Mhe.**	**Rashid Ali Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Kilimo,**

			Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Amani
16.	**Mhe. Hamad Rashid Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Afya / Uteuzi wa Rais**
17.	**Mhe. Maudline Cyrus Castico**	**-**	**MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais**
18.	**Mhe. Salama Aboud Talib**	**-**	**MBM/Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati / Nafasi za Wanawake**
19.	**Mhe. Sira Ubwa Mamboya**	**-**	**MBM/ Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais**
20.	**Mhe. Juma Ali Khatib**	**-**	**MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
21.	**Mhe. Said Soud Said**	**-**	**MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
22.	**Mhe. Khamis Juma Mwalim**	**-**	**Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe**
23.	**Mhe. Mihayo Juma N'hunga**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Jimbo la Mwera**
24.	**Mhe. Shamata Shaame Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Micheweni**
25.	**Mhe. Harusi Said Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete**
26.	**Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri**	**-**	**Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani**
27.	**Mhe. Mohamed Ahmada Salum**	**-**	**Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi**
28.	**Mhe. Chum Kombo Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale/ Nafasi za Wanawake**
29.	**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake**
30.	**Mhe. Lulu Msham Abdalla**	**-**	**Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Nafasi za Wanawake**
31.	**Mhe. Juma Makungu Juma**	**-**	**Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba , Maji na Nishati / Jimbo la Kijini**
32.	**Mhe. Hassan Khamis Hafidh**	**-**	**Naibu Waziri wa Biashara, na Viwanda /Jimbo la Welezo**
33.	**Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi**	**-**	**Naibu Waziri wa Kilimo,**

				Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mtopepo
34.	**Mhe.**	**Abdalla Ali Kombo**	**-**	**Jimbo la Mwanakwerekwe**
35.	**Mhe.**	**Ali Khamis Bakar**	**-**	**Jimbo la Tumbe**
36.	**Mhe.**	**Ali Salum Haji**	**-**	**Jimbo la Kwahani**
37.	**Mhe.**	**Ali Suleiman Ali (Shihata)**	**-**	**Jimbo la Kijitoupele**
38.	**Mhe.**	**Ahmada Yahya Abdulwakil**	**-**	**Uteuzi wa Rais**
39.	**Mhe.**	**Ame Haji Ali**	**-**	**Jimbo la Nungwi**
40.	**Mhe.**	**Amina Iddi Mabrouk**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
41.	**Mhe.**	**Asha Abdalla Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwengwa**
42.	**Mhe.**	**Bahati Khamis Kombo**	**-**	**Jimbo la Chambani**
43.	**Mhe.**	**Bihindi Hamad Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
44.	**Mhe.**	**Hamad Abdalla Rashid**	**-**	**Jimbo la Wawi**
45.	**Mhe.**	**Hamida Abdalla Issa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
46.	**Mhe.**	**Hamza Hassan Juma**	**-**	**Jimbo la Shaurimoyo**
47.	**Mhe.**	**Hidaya Ali Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
48.	**Mhe.**	**Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)**	**-**	**Jimbo la Mtoni**
49.	**Mhe.**	**Jaku Hashim Ayoub**	**-**	**Jimbo la Paje**
50.	**Mhe.**	**Khadija Omar Kibano**	**-**	**Jimbo la Mtambwe**
51.	**Mhe.**	**Machano Othman Said**	**-**	**Jimbo la Mfenesini**
52.	**Mhe.**	**Makame Said Juma**	**-**	**Jimbo la Kojani**
53.	**Mhe.**	**Maryam Thani Juma**	**-**	**Jimbo la Gando**
54.	**Mhe.**	**Masoud Abrahman Masoud**	**-**	**Jimbo la Bububu**
55.	**Mhe.**	**Miraji Khamis Mussa**	**-**	**Jimbo la Chumbuni**
56.	**Mhe.**	**Moh'd Mgaza Jecha**	**-**	**Jimbo la Mtambile**
57.	**Mhe.**	**Mohamed Said Mohamed**	**-**	**Jimbo la Mpendae**
58.	**Mhe.**	**Mohammedraza Hassanaali Mohamedali**	**-**	**Jimbo la Uzini**
59.	**Mhe.**	**Mtumwa Peya Yussuf**	**-**	**Jimbo la Bumbwini**
60.	**Mhe.**	**Mtumwa Suleiman Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
61.	**Mhe.**	**Mussa Ali Mussa**	**-**	**Jimbo la Ole**
62.	**Mhe.**	**Mussa Foum Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwani**
63.	**Mhe.**	**Mwanaidi Kassim Mussa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
64.	**Mhe.**	**Mwantatu Mbaraka Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
65.	**Mhe.**	**Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini**	**-**	**Jimbo la Dimani**
66.	**Mhe.**	**Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy**	**-**	**Jimbo la Chaani**
67.	**Mhe.**	**Nassor Salim Ali**	**-**	**Jimbo la Kikwajuni**
68.	**Mhe.**	**Omar Seif Abeid**	**-**	**Jimbo la Konde**
69.	**Mhe.**	**Panya Ali Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
70.	**Mhe.**	**Rashid Makame Shamsi**	**-**	**Jimbo la Magomeni**
71.	**Mhe.**	**Saada Ramadhan Mwendwa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
72.	**Mhe.**	**Said Omar Said**	**-**	**Jimbo la Wingwi**
73.	**Mhe.**	**Said Hassan Said**	**-**	**Mwanasheria Mkuu**
74.	**Mhe.**	**Salha Mohamed Mwinjuma**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
75.	**Mhe.**	**Salma Mussa Bilal**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
76.	**Mhe.**	**Shaib Said Ali**	**-**	**Jimbo la Chonga**
77.	**Mhe.**	**Simai Mohammed Said**	**-**	**Jimbo la Tunguu**
78.	**Mhe.**	**Suleiman Makame Ali**	**-**	**Jimbo la Ziwani**
79.	**Mhe.**	**Suleiman Sarahan Said**	**-**	**Jimbo la Chakechake**
80.	**Mhe.**	**Tatu Mohamed Ussi**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
81.	**Mhe.**	**Ussi Yahya Haji**	**-**	**Jimbo la Mkwajuni**
82.	**Mhe.**	**Viwe Khamis Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**

83.	**Mhe.**	**Wanu Hafidh Ameir**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
84.	**Mhe.**	**Yussuf Hassan Iddi**	**-**	**Jimbo la Fuoni**
85.	**Mhe.**	**Zaina Abdalla Salum**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
86.	**Mhe.**	**Zulfa Mmaka Omar**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
	Ndg. Raya Issa Msellem		**-**	**Katibu**

Kikao cha Ishirini na Saba – Tarehe 14 Juni, 2018

Kikao Kilianza Saa 3:00 Asubuhi

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Shehe Hamad Mattar) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha Mezani Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzei ya Zanzibar kwa mwaka wa Fedha 2015/2016 na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Mhe. Shaib Said Ali (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika): Mhe. Mwenyekiti naomba kuweka Hati Mezani kuhusu Hotuba ya Kamati ya (*PAC*) Kuhusu Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Naomba kuwasilisha Mhe. Mwenyekiti.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 15

Mgomo wa Wazee Charawe

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Miezi michache iliyopita kumeripotiwa kadhia ya baadhi ya wazee wa kijiji cha Charawe kuwazuwia watoto wao wasiende skuli, ambapo idadi kubwa ya watoto walitii maagizo hayo.

(a) Je, kulikuwa na matatizo gani yaliyosababisha hali hiyo.
(b) Je, ni hatua gani zimechukuliwa kutatua tatizo hilo.
(c) Je, ni viongozi gani walishiriki katika kutatua mzozo huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 15 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa katika kijiji cha Charawe baadhi ya wazee waliwahi kuwazuia watoto wao wasiende skuli ambapo baadhi ya wanafunzi walitii amri za wazazi wao.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub kama ifuatavyo:-

(a) Baadhi ya wazazi waliwazuia watoto wao wasiende skuli kutokana na mgogoro uliokuwepo baina ya wananchi wa kijiji hicho na Idara ya Misitu kutokana na kuzuiwa kukata msitu na kunyimwa vibali vya kusafirishia mkaa na kuni hadi hapo watakapofuata utaratibu uliowekwa na serikali. Hali hiyo iliwakasirisha wazazi na kuwazuia watoto wao wasiende skuli kwa kisingizio kuwa watoto wao wananjaa na wamekosa fedha za kuwanunulia chakula.

(b) Suala la kuwazuia wanafunzi kwenda skuli lilitatulia kwa mazungumzo ya pamoja na wananchi wa Charawe, yaliyowahusisha viongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Serikali ya Wanafunzi wa Skuli ya Charawe. Pia, Mkuu wa Mkoa Kusini Unguja aliunda Kamati ya watu wa Charawe ili kusimamia utatuzi wa suala hilo.

(c) Viongozi walioshiriki katika kutatua mzozo huo ni Mhe. Mkuu wa Mkoa Kusini, Unguja, Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Mkurugenzi Idara ya Elimu, Maandalizi na Msingi na viongozi kutoka Idara ya Misitu. Nawapongeza viongozi wote hao kwa jitihada na mashirikiano yao yaliyorejesha maelewano, ufahamu wa taratibu za serikali na kuleta amani na hatimaye watoto kurejea madarasani kujipatia haki yao ya msingi ya kupata elimu.

Pia, nawashukuru wananchi wa Charawe kwa usikivu wao na kuonesha mfano mkubwa kwa jamii nyingine katika kutoa mashirikiano yaliyopelekea kutatuka kwa mzozo huo. Napenda kuwashauri wananchi wa Charawe wasiwahusishe wanafunzi na migororo ambayo haiwahusu kwani kufanya hivyo kunaweza kuwanyima watoto haki yao ya msingi ya kupata elimu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize tu Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali masuala madogo sana ya nyongeza yenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Mwenyekiti, serikali imetafuta mbinu gani mbadala ya kuwatafutia chanzo cha kuendesha maisha yao kabla ya kuzuia ukataji wa mikoko ukizingatia mazingira ya wanaoishi wananchi hao hutegemea zaidi misitu. Lakini je, uongozi wa Chama Mkoa haukuingilia suala hili nao chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Ramadhan Abdalla Kichupa. *(Makofi).*

(b) Serikali ya Mkoa na Wizara ya Elimu ya Mafunzo ya Amali imechukuwa hatuwa gani za kukaa za wazazi na walimu kuwafundisha athari au madhara yale yalotokea. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekti, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Mwenyekiti, kuhusu mbinu mbadala ni kwamba mazingira ndio yanayoamua aina ya maisha watu waishi kilichofikiwa muwafaka ni kwamba lazima kuwa kuwe na matumizi endelevu yaliyopangwa na hili ndilo ambalo limefikiwa, wataendelea kuvuna lakini kwa utaratibu maalum ili kuona kwamba rasilimali iliopo pale inakuwa endelevu.

(b) Lakini pia pamoja na hivyo, kuna shughuli nyengine ambazo zinaweza kufanyika ikiwa ni pamoja na za uvuvi katika sehemu zile za Charawe. Vile vile, kuhusu kuwaelimisha wazazi na hata wanafunzi hili linaendelea kwamba katika ziara mbali mbali tunajaribu kuwaelekeza wananchi juu ya umuhimu wa elimu kwa vijana wao, na katika kufanya hivyo huwa tunafanya katika ziara, lakini pia Walimu Wakuu na watu wengine na Kamati za Skuli hufanya kazi hiyo na kwahili napenda kushukuru sana hasa Wilaya ya Kusini Unguja wako mbele katika suala hili. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuweza kuniona na kunipa nafasi katika majibu ya Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ametwambia kwamba mazingira ndio yanayoweza kuangalia hali halisi ya maeneo lakini tukiangalia mazingira ya Charawe ni msitu sasa sijuwi serikali imejipanga vipi ili kuona mbadala ya msitu na kuweza kuwasaidia wananchi wale. Nashukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, narejea kusema kwamba lazima rasilimali zilizopo katika jamii zitumike katika misingi ya uendelevu ili ziweze kutumika leo na kesho na kesho kutwa na kipindi kijacho, kilichofanyika pale ni kuweka utaratibu mzuri wa kuweza kumia msitu sehemu iliyohifadhiwa iheshimike lakini pia ilokuwa haijahifadhiwa itumike katika misingi mizuri hilo ambalo ndilo lililofanyika kwa mujibu wa mazingira yaliyopo.

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: kuhusu utaratibu Mhe. Mwenyekiti,

Mhe. Mwenyekiti: Taja Kanuni.

UTARATIBU

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Katika swali langu Mhe. Mwenyekiti, kwanza natumia Kanuni ya 37 swali nililoliuliza hajanijibu sasa sijui utaniruhusu niulize tena au vipi.

Mhe. Mwenyekiti: Kaa kitako kama kulijibu ameshalijibu kama hujaridhika..

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa ruhusa yako na busara ya kiti unisikilize ili na mimi niseme lile ambalo nimelikusudia.

Mhe. Mwenyekiti: Nimekuruhusu.

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali nimemuuliza swali wananchi wananchi wa Charawe mazingira yao ni msitu sasa katika kutokana na swali hili kuna njia gani ya mbadala ambayo imeandaliwa na serikali kuwasaidia wananchi wale katika kuendeleza maisha yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma naomba kurejea tena kusema kwamba njia mbadala ni kutumia misitu katika msingi wa uendelevu, sio kuleta viwanda vikubwa wala kuleta jambo jengine ni ile ile misitu kutumika katika misingi endelevu.

Nam. 176

Kuondoshwa kwa Madarasa ya Quran Maskulini

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Zamani katika skuli zetu kulikuwa na utaratibu wa madarasa ya Quran yakisaidia sana kuimarisha maadili ya vijana wetu wanapokuwa maskulini na katika jamii.

Je, kwanini utaratibu wa Madarasa ya Quran umeondoshwa na mbadala wake ni nini.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam 176 kama ifuatavyo: -

Utaratibu wa wanafunzi kupitia Madarasa ya Qurani katika skuli zetu umeondoshwa miaka mingi iliyopita, na badala yake yameanzishwa madarasa ya maandalizi ambamo ndani yake kuna somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu likijumuisha mada zote za somo hilo. Pia, somo la Dini ya Kislamu linafundishwa katika ngazi ya msingi na sekondari. Aidha, kumekuwa na ongezeko kubwa la vyuo vya Qurani ambapo wanafunzi pia hupata fursa kwenda kusoma Qurani baada ya saa za skuli au siku za mapumziko. Hivyo, palionekana kuwa hakuna haja ya kuwa na madarasa ya Qurani katika skuli. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kutosema hakuna haja yakuwa na mafunzo ya Qurani naomba kumuuliza maswali madogo ya nyongeza yenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali utafiti gani uliofanya kabla ya kuondosha mfumo uliokuwa ukitumika zamani hasa kwa kuzingatia mfumo wa endeshaji unaotumika hivi sasa umeshusha cha uelewa wa wanafunzi katika kiwango cha dini.

(b) Serikali haioni kuna haja ya kurejesha mfumo wa zamani hasa ukizingatia kuwepo kwa mmongónyoko wa maadili hasa ukizingatia watoto wetu wamekuwa wakiathirika kwa kukosa mila na desturi zetu na asilimia yetu karibuni 99 ni waislamu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba mfumo wa elimu Zanzibar ambao pia unajumuisha na baadhi ya masuala yanaohusu ya dini ya Kiislam ni kwamba mfumo huu ulifanyiwa utafiti na ukatumika na kulikuwa na sababu yake kwa nini yakaingizwa masomo ya Qurani katika skuli zetu ina historia ya muda mrefu tokea mwaka 1940 huko ilionekana kwamba ili kuwawezesha wananchi wetu kupata elimu hii ambayo labda tuiite ya kiskuli kulikuwa na haja ya kuingiza masomo ya dini, ili wananchi wetu kuweza kuelewa ili kuweza kuwapeleka watoto wao na ilitokana na kwamba wazazi wengi walikuwa wanasita kupeleka watoto wao kwa kuhufia kwamba labda wanaweza kubadilishwa katika misingi mingine ya dini. Kwa hivyo, kuweko somo la dini katika skuli za serikali ilikuwa ni kwa msingi huo, sasa baada ya uelewa kuwa mkubwa sana katika jamii yetu ikaonekana kwamba sasa hakuna haja ya kuweko jambo katika mfumo wa *Qurani Class* lakini yale yale masomo ya dini yanaendelea kusomeshwa katika maandalizi, msingi na sekondari hio hasa ndio sababu ya msingi.

Kwa hivyo, kutokana sasa na kuwepo madarasa nyingi, vyuo vingi kila pahali sisi elimu tumebakisha na kusomesha tu masomo ya dini katika ngazi zote za maandalizi, msingi na sekondari.

(b) Na kuhusu kushuka kwa mafunzo ya dini hapana sasa hivi mafunzo yako zaidi kuliko wakati mwengine uliopita kutokana na kuongezeka kwa idadi kubwa ya wasomi ambao wanapitia mfumo wa serikali ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuna kundi la watu ambao sasa hivi wanasoma masomo ya dini katika vyuo vyetu vya ndani na nje. Kwa hivyo suala hilo lipo wala mafunzo ya dini bado hayajazuiliwa skuli, ispokuwa yapo katika mfumo mwengine unaoendelea. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu utaratibu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante kuhusu utaratibu

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoubu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilichomuuliza Kanuni ya 37 haina haja ya kusoma nimemuuliza tu Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali

Mhe. Mwenyekiti: Endelea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante serikali haioni kuna haja ya kurejesha mfumo huu ilikuwa anijibu tu ipo haja hakuna haja.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub nimeeleza kwa urefu lakini yeye mwenyewe alitaka niseme ndio au hapana narejea nilivyosema kwamba sababu ya kuweko somo hili ilitokana na uwelewa mdogo wa wanachi wetu juu ya elimu ya kizungu na ndio maana tukaingiza sasa baada ya uelewa ule kuwa mkubwa sasa hakuja ya kuweko *special class* ambayo tunaita *Qurani Class* badala yake masomo ya dini yanaendelea vile vile ndani ya skuli ya nje ya skuli. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Nam. 123

Kupata Kuku wa Kisasa katika Kisiwa cha Pemba

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:

Katika visiwa vya Zanzibar hasa Pemba kuna tatizo la kitoweo cha kuku wa kisasa kutokana na tatizo la kiwanda cha kutoa vifaranga vya kuku na chakula chake ambapo vitu hivi vinapatikana Tanzania Bara. Na kwa sababu kisiwa cha Pemba pamoja na kuwa kuna wafugaji wa kuku wa kienyeji, lakini bado ipo haja ya kupata kuku wa kisasa kwa bei rahisi.

(a) Je, serikali inalijua hilo na kama inalijua imechukua hatua gani.

(b) Je, kuna mpango wa karibu wa dharura wa kuleta kiwanda cha kutoa vifaranga na chakula chake.

(c) Je, inagharimu kiasi gani kwa kiwanda cha kutoa vifaranga kitaalamu na kiwanda cha chakula.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi – Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa ya kujibu maswali yaliyoulizwa na Mhe. Suleiman Sarahan Said lakini kwanza kabla sijajibu swali naomba nitowe pongezi zifuatazo utaniruhusu.

Mhe. Mwenyekiti: Endelea Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Kwanza leo Mhe. Mwenyekiti, ikiwa ni mwezi 29 Ramadhani ambapo tunategemea kama utaandama baada tu masaa pengine machache niseme tutakuwa na Baraza la Iddi nawapongeza Waislamu wote kwa mufunga kwa salama na amani. Pili nampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jitihada zake anazozichukuwa katika kuingoza nchi yetu kwa kweli mafanikio tuliyopata ni mengi ukiangalia katika sekta za mawasiliano unaona barabara, usafiri wan chi kavu umeimarishwa, usafiri wa baharini umeimarika hata ukiangalia nyuma kama miaka 10 iliyopita utaona tofauti kati ya miaka ile na hivi sasa hata idadi ya magari unaiona imeongezeka, barabara zinatanuliwa, majengo yanajengwa, meli zimekuja nakadhalika nakadhalika kwa kweli ni maendeleo makubwa sana, napenda kutoa pongezi zangu za dhati.

Mhe. Mwenyekiti, zaidi ya hayo Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein ameweza kutuongoza katika hali ya mshikamano mkubwa sana, ameweza kutuongoza katika hali ya umoja mkubwa sana, ameweza kutuongoza pia katika hali ya ushirikiano mkubwa sana nchi yetu imekwenda kwa salama na amani tunashukuru sana.

Pia nimpongeze Makamu wa Pili wa Rais ...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Naibu Waziri endelea na majibu muda umekuwa mwingi endelea.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante Mheshimiwa nakubaliana na mawazo yako.

Sasa niingie kwenye kujibu maswala, Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said jembe Mwakilishi mahiri huyu swali yake lenye kifungu a, b na c kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Mwenyekiti, serikali inakubaliana na Mjumbe kuhusiana na uchache wa viwanda vya kutotolea vifaranga na utengenezaji wa chakula cha kuku wa kisasa. Kwa kulifahamu hilo, serikali imekuwa ikishajiisha sekta binafsi kuanzisha viwanda vya namna hiyo kwa lengo la kujiinua kimaisha pamoja na kutoa ajira kwa wananchi wengine. Aidha, serikali inaendelea kutoa taaluma kwa wafugaji na wafanyabiashara wengine juu ya namna bora ya kusimamia na kuendesha sekta hii.

(b) Mhe. Mwenyekiti, hatua zilizochukuliwa na serikali za kushajiisha sekta binafsi kuanzisha viwanda vya chakula na vya kutotolea vifaranga vya kuku zimeanza kuonyesha mafanikio kwa kuanzishwa viwanda vidogo vidogo vya kutengeneza chakula cha kuku na kutotolea vifaranga.

(c) Mhe. Mwenyekiti, gharama za mashine au kiwanda hutegemea na ukubwa na aina ya mashine zinazotumika ambazo huuzwa kwa bei tofautiana pia . Kwa mfano, mashine ya kutotoa vifaranga 100 huuzwa kwa wastani wa shilingi laki nne (400,000/=) za na mashine ya kuchanganyia chakula cha kuku tani moja na nusu huuzwa kwa wastani wa shilingi milioni kumi (10,000,000/=) bila kuchanganya gharama ya jengo na malighafi ya kutengenezea chakula cha mifugo ambavyo hivi pia vinatafautiana sana. Hivyo, gharama hutegemea na ukubwa wa kiwanda pamoja na mashine.

Mhe. Mwenyekiti, serikali inaendelea na jitihada za kutafuta wawekezaji wa kuzalisha vifaranga na kujenga kiwanda cha chakula cha mifugo, ili kuziba pengo la uhaba mkubwa wa bidhaa hizo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Ingawa mimi ni tafauti na wenzangu sana lugha za humu ndani ambazo mimi huyu shemegi yangu, rafiki yangu, nani yangu sipendi napenda yule nimwite Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugu na Uvuvi ingawa ni shemegi yangu rafiki yangu. Lakini nasema sipendi, napenda cheo alichopewa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, yeye ni Mhe. Naibu Waziri akijibu kwa niaba ya Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumzie kwamba kutokana na tatizo ambmalo tunali la uhaba wa chakula kwa kuzalisha ndani ya nchi kuku tunao wa kienyeji lakini kwa minasaba ya kisasa ni kwamba kuku anachukuwa muda mrefu kwa ajili ya kumpata kuku anachukuwa muda wa miezi sita mpaka mwaka ndio kuku uweze kumla na ndio tukatayarisha au mitaala mingine ikatayarisha kuku hawa wa kisasa ambao wanachukuwa mwezi mmoja kwa kula.

(a) Sasa nimuulize Mhe. Naibu Waziri kwamba kwa kuwa muda mrefu sana serikali imeshatoa agizo hili la kuwapa wawekezaji waweze kufanya kitu hichi ambacho na Zanzibar kwa sasa hivi ni chakula adhibu sana chips kuku na kinachotumika sana. Lakini mpaka sasa hivi sekta hii ya uwekezaji katika sekta ya mifugo bado haijakamilika. Je, Mhe. Waziri ananambiaje kuhusu suala la kuanzisha kiwanda ambacho kitakuwa mfano wa wawekezaji au wananchi au wawekezaji wa ndani, ili waweze kukiiga kiwanda kile au waweze kushajihisha kwa sababu wawekezaji wameshindwa kujiwekeza wenyewe.

(b) Watu wengi wa uvuvi tulishindwa kuekeza katika sekta ya uvuvi na serikali imeamua sasa hivi kurudisha tena hili Shirika la Uvuvi na kuweza kuunda boti na kila kitu. Je, serikali imejipangaje kwenye suala la mifungo katika sekta ya kuku, kutotoa pamoja na chakula chake.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikiri kwamba suala la viwanda liko chini ya Wizara ya Biashara na Viwanda lakini kwa sababu swali alilouliza lina mnasaba na Wizara ya Kilimo basi nitamjibu kama ifuatavyo:-

(a) Nakubaliana na Mjumbe alaiposema kwamba tuanzishe kiwanda cha mfano na kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara na Viwanda tutajadiliana namna ya kukiweka kiwanda hicho cha mfano kwa sababu nakumbuka kilikuwepo kiwanda cha kutotoa vifaranga pale kikiendeshwa na serikali na kilitosheleza kabisa mahitaji ya ndani. Lakini kilipobinafsishwa kiwanda kile tukampa mtu binafsi naye mwanzo alienda vizuri sana lakini hatiame baadae alikuja aka- *collapse* akawa hakuweza tena kuzalisha vifaranga na hivyo, jengo lile likakodishwa na Wizara ya Biashara na Viwanda likafanywa *store*.

Sasa hivi Wizara ya Biashara na Viwanda italitumia jengo lile katika mfumo wao wa kuendeleza viwanda watalitumia jengo lile ili kuendeleza viwanda.

(b) Namna ilivyojipanga wizara kuimarisha hiyo mifugo kwa kutumia hivi viwanda vidogo vidogo. Kwa kweli, hapa Zanzibar sasa hivi tunazalisha chakula cha kuku na kuna wawekezaji wakubwa ambao wanasafirisha chakula cha kuku kutoka hapa Zanzibar kupeleka Bara na mmoja wao ni huyu anaitwa Bin Shuwari anatengeneza chakula cha kuku hapa na anasafirisha kule Pemba. Lakini tunakiri kwamba hakijatosha na wapo wengine wengi ambao wanafanya hivyo, kuna hata wale binafsi wakulima ambao kwa kweli wanatengeneza vyakula vya kuku kwa ajili ya kuku wao na ziada wanauza nje.

Kwa hivyo, watu binafsi tunaendelea kuwahamaisha lakini wakati huo huo narudia kusema kwamba tutachukuwa wazo lake turudishe kiwanda cha mfano, ili wale wawekezaji waweze kuiga namna ya kutotoa viranga na kuzalisha chakula cha kuku. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Machano Othman Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi naomba kuulizwa swala a na b kama ifuatavyo:

Wakulima wengi wa Zanzibar wakiwemo wafugaji wamevunjika moyo sana katika sekta ya mifugo kutokana na nchi kuruhusu uingizaji wa kuku kutoka nje na samaki kutoka nje na kuwafanya bei kuwa ndogo na wakulima na kuendeleza katika shughuli hizi.

(a) Kwa kuwa nchi zote za Afrika Mashariki haziruhusu kuingiza kuku kutoka nje na samaki. Je, serikali haioni kwamba baada ya kuingiza kuku wangeliwaomba wawekezaji kuja kuweka viwanda vya kuzalisha kuku hapa ili kupata kazi na ajira wananchi. Serikali ina kauli gani kuhusu uingizwaji wa kuku kutoka nje ya nchi.

(b) Kiwanda cha chakula cha kuku cha *ZAPOCO* ambacho kilibinafsishwa pale Maruhubi baadae Serikali ya Mapinduzi ya awamu wa saba ilikubaliana na waliokuwa wamebinafsishiwa kukirejesha serikalini na kulipwa fidia na hatua hiyo nafikiri imefanyika. Lakini hadi leo kiwanda kile kimekuwa ni ghala la kuweka saruji. Ni lini kiwanda kile kitarejea tena katika uzalishaji wake au kufanyika shughuli nyengine za kiserikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Mwenyekiti, suala la uingizaji wa kuku hapa nchini kwa kweli sote hatulipendi tunajua hivyo, lakini suala hili lilikuja likakubalika kwa sababu ya upungufu wa kitoweo hichi cha kuku na sasa hivi tunavyoshajihisha watu wetu wafuge kuku hawa wa kisasa ni mategemeo yangu kwamba hii biashara ya kuku iyayukoa hawa kuku wa nje hawa wanaoitwa Peduu hawa itayayuka na itapotea kabisa. *(Makofi)*

Nakumbuka hapa tena narudi *ZAPOCO* walipokuwa wanazalisha kuku pale ilikuwa wanauza kuku pale ukienda saa yoyote ukienda unanunua unaondoka na waliweza kuuza hata vifanga nje.

Kwa hiyo, tutahamaisha na kama nilivyosema mwanzo kwamba tutafanya hivyo alivyotushauri Mhe. Suleiman Sarahan Said kwamba tuanze kiwanda cha mfano kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara. Basi nadhani tatizo hili la kuleta chakula cha kuku litatoweka wenyewe kwa sababu hata wananchi hawapendi kula kuku hawa wa Peduu.

(b) Kuhusu suala lile kutumika kuweka saruji. Nilisema mwanzo kwamba baada ya *ZAPOCO* kushindwa kuendeleza kiwanda kile jengo lile lilikuwa tupu. Kwa hivyo, Wizara nadhani ya Fedha walilikodisha jengo lile kwa mtu binafsi na akaweka saruji. Lakini sasa hivi Wizara ya Biashara na Viwanda inalishughulikia jengo lile kuweza kuweka kiwanda pale cha uzalishaji.

Kwa hiyo, mambo mawili yatakwenda sambamba pale kutakuwa na kiwanda ambacho Wizara ya Biashara na Viwanda itaamua na sisi huku tunatafuta njia ya kufanya kiwanda cha mfano ambacho kitatoa vifaranga vya kuku. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri aliyoyajibu sasa kuhusu suala hili ambalo ni muhimu sana lililoulizwa na Wajumbe kama watatu hivi. Ningeomba kutoa majibu ya ziada kwa ajili ya kuwa sote tuondoke tuwe na msimamo mmoja.

Mhe. Mweyekiti, kama unakumbuka huko nyuma Sera ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilibalidika, serikali ilijitoa kuendesha viwanda baada ya kuona viwanda walivyokuwa navyo nyuma kimkakati tukaona kwamba ijitoe kuendesha viwanda. Lakini pia Sera ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni kuhakikisha kwamba tunashirikiana vizuri sisi kama serikali na sekta binafsi na ndio maana kukawa kuna sera na kuna sheria ile ya *PPP*.

Sasa kuhusu suala zima la kiwanda cha kutotoa kwa kuku, suala hili limo katika programu ya kushajihisha viwanda ambayo bajeti yake tumepatiwa hivi sasa, tunashajihisha wafanyabiashara binafsi na viwanda vya nje vije kujenga kwa ajili sekta hiyo, kwa sababu tunataka vitosheleze sio tu wananchi wa Zanzibar lakini pia Sekta ya Utalii ambayo inachukuwa sehemu kubwa kutumia vifaa vinavyotokana na kuku.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, lililoulizwa kuhusu eneo la *ZAPOCO* niseme tu kwamba lile eneo ndio limepewa na serikali wizara yetu kwa ajili ya kuweka Makamu Makuu ya *SMIDA* na sasa hivi bajeti tumepewa kama bilioni tatu kwa ajili ya kufanya kazi hiyo. Lakini bado msimamo wa kuwa na kiwanda cha kutengeneza chakula cha wanyama wakiwemo wanyama kama kuku na wanyama wengine imo katika programu yetu na wawekezaji tunazungumza nao na mara kwa mara tushazungumza na wachina na watu wengine wanaokuja ili waweze kuweka hapa.

Tatizo kubwa liliopo hapa Zanzibar wapo watu binafsi wanaofuga kuku na wanatotoa kuku vifanga. Tatizo lililokuwepo ni kwamba huwa wanashindana sana na vifaranga vinavyotoka nje hata mayai yanayotoka nje, kuna malalamiko sana kwamba kulifika wakati mayai na viranga vinavyotoka vikawa vinaumiza soko la ndani. Jambo hilo tunalitizama na mmoja ambayo tumekubaliana na serikali kwamba kulinda viwanda vyetu vya ndani na kuwalinda wakulima wetu.

Kwa hiyo, ningewaomba Waheshimiwa Wawakilishi wajue tu kwamba tuko vizuri, lakini mchakato unaendelea na in sha alla tutapata kushajihisha viliomo hapa ndani. Uwezo huo

tunao Mhe. Mwenyekiti, najua mie kuna wafugaji sasa wanatoa mayai zaidi ya elfu sita mpaka elfu kumi wapo hapa Zanzibar, uwezo huo upo tuwashajehishe wafanye kazi zaidi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na kwa umuhimu wake suala hili na kwa umuhimu wa wafugaji wetu wa Zanzibar naomba nichukuwe fursa hii kuongezea sehemu ndogo ambayo pamoja na majibu mazuri aliyoyajibu Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda na kuweka wazi suala hili kidogo amelisahau na nampongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri aliyoyatoa pamoja na ufafanuzi mzuri ambao kautoa Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli suala hili linagusa sana wafugaji ambao ni sehemu kubwa ya wananchi walio wengi Zanzibar na hujitafutia ajira na kipato chao hapa Zanzibar. Nataka niwaeleze tu kwamba eneo ambalo lililokuwa linatumika na *ZAPOCO* lililokuwepo Kizambani mbali ya lile ghala lililokuwa likitumika pale eneo lile lipo katika mikono ya serikali na wamepewa Wizara ya Kilimo kwaajili ya kulitumia kama ni eneo la utafiti.

Kwa hiyo, mbali ya kuongeza vile viwanda vidogo vidogo kama tunavyosema sasa hivi tuna *SMIDO* na *SMIDO* ndio waliopewa lile eneo la ghala za *ZAPOCO* sera haitawapa tena watu wa kawaida kuendesha yale masuala ya maghala na maeneo ambayo serikali inamiliki.

Kwa namna hiyo basi lile eneo liliokuwa likitumika katika kufuga kuku pale Kizimbani litaendelea kuwa ni eneo la kufanyia tafiti za mifugo wakiwemo hao kuku na wanyama wengine na hivi sasa hatua iko mbali zaidi katika kulifanyia kazi.

Vile vile, nataka niwajuilishe wananchi kwa ujumla wao kweli wizara ina jukumu la kusimamia bidhaa zote zinazotokana na mifugo ambazo zinatoka nje ya nchi. Kuanzia bajeti hii ambayo tunaishughulikia tutakuwa na usimamizi mkali kabisa ili kuhakikisha kwamba tunalinda wananchi wetu wanaofuga hapa na wanaovua hapa na kuzilinda zile biashara zao na kuhakikisha kwamba biashara zinazotoka nje ama zitaongezwa kodi ili ziweze kupambana na hali halisi ya hapa. Lakini vile vile kutakuwa na ada maalum ili kuweza kuwalinda wale wafugaji wetu. Kwa hivyo, hilo litaanza hivi karibuni tutapoanza mwezi wa Julai. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Nam. 198

Ukosefu wa Vitendea kazi Mamlaka ya Maji Wilaya ya Micheweni

Mhe. Shaib Said Ali (Kny. Mhe. Omar Seif Abeid) – Aliuliza**:**

Kabla ya kujibiwa naomba kidogo kwa niaba yake tena nifanye marekebisho kama ifuatavyo:

Kuna tatizo la mabadiliko ya mishahara kwa wafanyakazi wa *ZAWA* kwa niaba yake kifungu hiki kaniomba nikiondoe, na pia swali la (c) kaniomba niliondoe. Kwa hivyo, maswali yaliyobakia naomba waziri anijibu. *Inshaallah* ahsante.

Kwa kuwa mafundi wa Mamlaka ya Maji ya Wilaya ya Micheweni wanakabiliwa na usumbufu wa vitendea kazi sambamba na tatizo la usafiri kutokana na uhalisia wa Kijiografia ya Wilaya ya Micheweni.

(a) Je, Mamlaka ya Maji Pemba ina mpango gani na lini watawapatia vitendea kazi vipya mafundi kama vile spana za kuanzia namba 3 na kuendelea ambazo ndio muhimu kwa ajili ya kufungia viungo vya mabomba hayo.

(b) Je, *ZAWA* wana mpango gani wa kuwapatia vyombo vya usafiri mafundi bomba na fundi umeme wa Mamlaka wa Wilaya ya Micheweni, ili waweze kufanya kazi zao kwa uhakika.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati - Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa idhini naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam.198 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Lakini kabla ya kujibu naomba niweke sawa jambo ambalo Mhe. Mjumbe kalisema, ni kwamba nilimuomba arekebishe jambo la majibu kwenye kipengele cha c. Jana nilizungumza na uongozi wa Baraza baada ya jawabu sahihi lakini baada kufungua *order paper* nimekuta kidogo imerejewa kwa hivyo nilimuomba jawabu sahihi ndio alibakishe baada ya hayo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Maji Pemba ina mpango wa kununua vifaa vya ukubwa tofauti kwa Afisi zake za Wilaya zote za Pemba kila inapotokea haja ya kufanya hivyo. Aidha, kwa mara mwisho tarehe 5/3/2018 Afisi ya Maji ya Micheweni ilipatiwa vifaa vifuatavyo:-

Spanner moja moja aina ya *Fix* za ukubwa wa inchi 24/26, 22/20, 25/28, 21/23, 24/27,18/19, *pipe wrench* 6 za inchi 4 na *pipe wrench* 6 za *inch* 18.

(b) Mhe. Spika, *ZAWA* Afisi ya Pemba inakiri kuwepo kwa upungufu wa vyombo vya usafiri kwa Afisi zake zote za Wilaya za Pemba. Kutokana na upungufu huo, magari yaliyopo yanatumika kulingana na matatizo yanavyojitokeza katika wilaya husika. Aidha, kwa hatua za awali *ZAWA* imenunua piki piki moja kwa ajili ya Afisi ya Maji ya Micheweni ili isaidiane na vespa iliyoko kwa lengo la kupunguza makali ya upungufu wa usafiri kwa mafundi wake wa bomba na umeme. Vile vile, utaratibu wa kupeleka gari kubwa hufanyika kila inapotokea haja inayolazimisha kufanya hivyo.

(c) Ni kweli kwamba Mamlaka ya Maji bado haijapokea mishahara mipya tangu ulipotangazwa lakini wafanyakazi hao wataanza kulipwa kuanzia Julai, 2018.

Mhe.Shaib Said Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali dogo kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, tatizo hili la upungufu wa vifaa katika wizara yako sio Pemba peke yake au Wilaya ya Micheweni peke yake ni Wilaya zote za Unguja na Pemba. Je, wizara yake ina mpango gani

au ina dhamira gani mahsusi ya kuwafanyia wananchi hawa au wafanyakazi hawa wapate vitendea kazi, ili kurahisisha kazi zao na kuleta ufanisi katika wizara hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Mwenyekti kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Shaibu Said Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Hiyo ni dhamira halisi ya Mamlaka ya Maji Zanzibar kwa sababu lengo letu la msingi ni kuwafikishia wananchi maji sasa nyenzo zote muhimu za kuhakikisha kwamba wafanyakazi wetu wanafanya kazi vizuri kwa kutimiza lengo ndio azma yetu kufanikisha. Hivyo basi ni azma yetu ya kuhakikisha kwamba tunapata vifaa vyote vinavyohitajika kwenye ofisi zetu za *ZAWA* Unguja na Pemba.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nikishukuru sana kwa kuniona lakini vile vile nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri leo ambayo yametulia sana. Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka kujua kwa kuwa tangu ilipotangazwa mishara mipya ya makampuni na taasisi na serikali yafika sasa takriban mwaka. Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri mbele ya Baraza lako tukufu hivi karibuni watalipwa mishahara yao. Je, katika kile kipindi ambacho hawakupata mishahara yao serikali inatamka tamko gani kutoa pesa zao za *area* kwa wale waliobaki tokea kipindi kile hawajatiliwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mohammed Said Mohammed swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kama itakumbukwa ni kwamba suala hili liliibuka wakati wa hutuba ya bajeti ya wizara yetu na lilitolewa ufafanuzi lakini kwa bahati mbaya tu Mhe. Mohammed Said Mohammed hakuwemo kwenye Baraza wakati ule ndio maana hakupata kulisikia lile jawabu.Lakini ni kwamba Wizara ya Katiba Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Wizara yangu ya Ardhi, Nyumba Maji na Nishati watakaa kuangalia utaratibu na kutazama namna muafaka juu ya jambo hilo ilizungumzwa vya kutosha na nisingependa kulirejea tena.

Nam. 115

Kupata Vifaa vya Kutunzia Karafuu

Mhe. Shaib Said Ali (Kny. Mhe. Omar Seif Abeid) – Aliuliza:

Shirika la Taifa la *ZSTC* ndio lenye dhamana ya kununua karafuu Zanzibar ambayo inaongoza kwenye soko la dunia kwa ubora wake. Kwa kuwa shirika linahitaji kuwapatia vifaa vya kutunzia Karafuu wakulima kama vile majamvi, kapu, pishi na nyenginezo, kwa wachumaji na kuwepo kwa mashine za kusafishia karafuu na magunia.

(a) Je, pamoja na kukopesha fedha za kuchumia karafuu, kuna utaratibu gani wa kuwakopesha vitendea kazi wakulima wa karafuu, ili kuhakikisha kwamba karafuu zote zinaanikwa kwenye majamvi na kupata karafuu nyingi zaidi zenye daraja la kwanza.

(b) Je, kwenye msimu huu wa uchumaji wa karafuu uliopita, shirika lilinunua karafuu kiasi gani za daraja la kwanza.

(c) Je, kuna utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba karafuu zinahifadhiwa kwenye magunia badala ya ule uliopo hivi sasa wa kuhifadhi karafuu kwenye mapolo ambayo hupelekea karafuu kusinyaa na kupoteza uzito na rangi yake ya asili.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake Nam. 115 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Shirika limekuwa na kawaida ya kutenga fedha kwa ajili ya kuwakopesha wakulima wa zao la karafuu kwa ajili ya maandalizi ya mwanzo ya uchumaji wa karafuu kwa ajili ya maandalizi ya mwanzo ya uchumaji wa karafuu na kutakiwa kuzirejesha fedha hizo ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya kukopeshwa. Aidha, shirika limekuwa na utaratibu wa kukopesha vifaa vya vuno kama vile majamvi na pishi kwa masharti maalum ya kurejesha fedha hizo kabla ya msimu kwisha.

(b) Kwa msimu huu wa 2017/2018 hadi kufikia tarehe 30/04/2018 shirika limeshanunua kiasi ya tani 8292.2 za daraja la kwanza zenye thamani ya shilingi 116.09 bilioni kwa bei ya kununulia karafuu daraja la kwanza kutoka kwa mkulima ni shilingi 14,000.00 kwa kilo moja kwa msimu huu.

(c) Shirika limeendelea kuwaelemisha wananchi juu ya njia sahihi na bora ya uchumaji, uanikaji na uhifadhi wa karafuu ili kulinda ubora wa karafuu zetu za Zanzibar ikiwemo kuhifadhi karafuu hizo katika magunia maalum.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuumuliza swali moja la nyongeza. Kwanza naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuwapa wakulima asilimia 80 ya bei ya soko la dunia. Kwa hivyo, naipongeza serikali kwa jambo hilo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nimulize Mhe. Waziri kwa kuwa bei ya shilingi 14,000.00 imedumu kwa muda mrefu sana hapa Zanzibar kwa wakulima kuuza bei hiyo kwa zao la karafuu kwa daraja la kwanza. Je, namuuliza Mhe. Waziri kwa msimu ujao awaeleza nini wakwezi na wakulima wa nchi hii kuhusu habari ya bei itaongezeka au itabakia hapo hapo.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mussa Foum Mussa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda na yeye kumpongeza kwa kuthamini na kuzitambua juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuipongeza serikali dhidi kuwapa wananchi asilimia 80 ya mapato ya karafuu. Kwa hivyo, napenda sana kumpongeza na kumshukuru kwa kutambua juhudi za serikali. *(Makofi)*

Lakini swali lake je, bei ya shilingi 14,000.00 imekaa kwa muda mrefu je msimu ujao itaongozeka na au laa. Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba na yeye atambue juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wa awamu ya saba kwa kuzipandisha bei ya karafuu juu sana. Mhe. Mwenyekiti mwaka 2010 tulipoingia katika serikali amau ya saba karafuu zilikuwa zinauzwa shilingi 3500 mara tu baada ya kuingia Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein karafuu ziliongezwa bei hadi kufikia 14,000.00 kwa kilo daraja la kwanza.

Kiasi ambacho wananchi wote wanafurahi na wanapendezwa na bei hiyo. Lakini naomba kumwambia itapobidi na ikiona serikali inahitaji kuwaongezea bei juu ipande serikali haitosita kufanya hivyo kwa sababu serikali ndio jukumu lake katika kuwatafutia maendeleo wananchi wake.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa wasaa huu kuuliza swali moja dogo la nyongeza, nampongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri anayotupatia namuomba kumuliza swali moja tu lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Ni asilimia ngapi ya karafuu zinazonunuliwa *ZSTC* ziko katika daraja la kwanza na la pili.
b) Je, shirika linatoa *motivation* gani kwa wakulima wale wanaozalisha karafuu nyingi katika daraja la kwanza.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame swali lake lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Asilimia ngapi zinanunuliwa daraja la kwanza. Ukisoma katika jibu langu mama kwamba bei tunayonunua 14,000.00 kwa kilo daraja la kwanza lakini asilimia ngapi kwa kweli ukiangalia kiwango ile *exactly* asilimia kwa sasa hivi sitoweza kukupatia nitakupatia kwa maandishi. Lakini ninachotaka kukwambia ni kwamba asilimia kubwa ya karafuu tunazozinunu *ZSTC* tunazinunua daraja la kwanza, kwa sababu ya kuwaeleimisha wananchi wetu juu ya kuzichuma kuzihifadhi na hadi kuziuza, ili wananchi wetu wapate karafuu za daraja la kwanza wapate pesa iliyokuwa nzuri zaidi.

Swali la pili ningeomba kidogo arudie sikumsikia.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Swali la pili. Je, shirika linatoa *motivation* gani kwa wakulima wanaozalisha karafuu nyingi katika daraja la kwanza.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Mwenyekiti, naomba kujibu swali b kama ifuatavyo:-

Serikali tunatoa motisha kwa wananchi kulilima zao la karafuu kwa sababu ya thamani yake na ubora wake wa zao zima la karafuu la Zanzibar. Sasa daraja la kwanza, daraja la pili na daraja la tatu lakini *point* ni kwamba serikali inatoa *motivation* ya kila aina kwa mfano kuwakopesha

wakulima majamvi, kuwakopesha pesa, kuwafanyia mambo mbali mbali ili waendelee ili waendelee kulilima na tupate karafuu za daraja la kwanza kwa sababu ndio lenye soko la juu zaidi na wao wananchi waweze kupata pesa iliyobora kwa sababu daraja la kwanza kama nilivyosema bei yake ni shilingi 14,000.00. Kwa maana hiyo, tunahakikisha wananchi wetu tunawaelimisha tunatoa motisha waweze kupata karafuu daraja la kwanza wawezekutuuzia.

Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nitoe nyongeza kumjibu Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini, ni kweli katika uchumaji wa karafuu serikali kupitia *ZSTC* huwa inawapa zawadi wakulima wale ambao wanauza karafuu nyingi lakini pia wanauza karafuu *grade* ya kwanza. Tunatoa zawadi kwa viwango mbali mbali nakumbuka mimi mwaka juzi Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein alishiriki kuweza kutoa zawadi kwa mkulima bora wanaitwa wakulima bora, na utaratibu huu tutaendelea nao kufanya hata mwaka huu na miaka mingene ijayo ili iwe motosha kwa wale wote ambao wanauza nyingi sana *ZSTC* kama mnavyojua kwamba wengi zamani wakikimbia kuuza *ZSTC* lakini wanauza *ZSTC* kwa wingi lakini pia grade ya kwanza.

Nam. 165

Kutofata Utaratibu wa Gari Zinazoingia Nchini na Kuruhusiwa Kuendeshwa Bila ya Vibali

Mhe. Suleiman Sarahan Said: - Aliuliza:

Katika kutekeleza majukumu yake ya miundombinu ya bahari na nchi kavu kuna tatizo ambalo linaonesha kama halifuati utaratibu kama vile gari inapoletwa kwa meli kuingia nchini gari hiyo haina leseni wala bima na huruhusiwa kutembea barabarani, ili kuenda sehemu alipo muhusika wake, lakini gari hiyo hupakiwa mizigo mengine mpaka wakati mwengine haiwezi kutembea kwa kawaida.

(a) Je, serikali inalijua hilo.

(b) Je, ni ruhusa kupakia mizigo gari inayotoka bandarini.

(c) Je, kama kutatokea ajali ambayo itasababishwa na gari inayotoka bandarini ambayo ndio kwanza kinaingia nchini nani atakuwa muhusika.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi Suleiman Sarahan Said swali lake Nam. 165 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha Sheria nambari 7 ya mwaka 2003 *"Road Transport Act"* kinatoa ruhusa gari inayoingia nchini kutembea barabarani bila ya kusajiliwa kwa masharti kwamba gari hiyo inatembea kwa kuendeshwa ili kupelekwa kwa muhusika.

(b) Si ruhusa gari kufanya kazi ya kupakia abiria au mizigo kupakia kwa sababu ruhusa ya kupakia mizigo na abiria inatolewa baada ya gari husika kukaguliwa na kuonekana inafaa kutekeleza majukumu hayo.

(c) Kama ajali imesababishwa na gari inayotoka Bandarini dereva wa gari husika ndie atakaekuwa muhusika wa ajali hiyo na atachukuliwa hatua za kisheria kwa mujibu wa kosa alilolifanya na kusababisha ajali.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimshukuru waziri kwa majibu yake mazuri sana ambayo wengine wanamwita *Iron Lady* lakini mimi sipendi namwita Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Sasa nimuulize swali la nyongeza, kwamba nakubaliana naye katika majibu yake lakini mara nyingi tulikuwa na mazoea hapo siku za nyuma kwamba watu maalum ndio walikokuwa wakilite gari na zilikuwa zikifikia mjini sasa hivi gari kila mmoja anauwezo wengine wanaka Makunduchi wengine wanakaa maeneo mbali sana ambayo Nungwi ambayo *more than* 56 *kilometres* inakwendwa katika mazingira ambayo siyo na wakati huo huo gari ile wakati wameleta anapakia na mzigo wake ndani.

Lakini Mhe. Waziri ananiamba hapa kwamba tayari kuna sheria ambayo inamlinda yule mtu kutembeza gari lake mpaka kule, sasa hatakiwi alivyoniambia kubeba ule mzigo lakini ikitokea gari lile mathalan limemgomga mtoto na gari lile halina *insurance* ingawa waziri anasema kwamba mtu yule atawajibika mwenyewe. Kwa hivyo, hapa namuomba Mhe. Waziri anipe maelezo inakuwaje katika kifungu hichi cha sheria na wakati huo yule dereva kinamlinda lakini sasa barabara pamoja na askari kutokana na kesi inamlindaje kuhusu *insurance*, ninachokitafuta pale *insurance* ya mtoto yule kwa sababu gari haina *insurance* ataipataje haki yake.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, katoa maelezo mengi mpaka swali limekuwa haliko *clear,* naomba swali alifanye liwe fupi ili nijue nini cha kumjibu.

Mhe. Mwenyekiti: Rudia swali lako kwa ufupi ili waziri aweze kukujibu, nenda moja kwa moja.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nimemfahamu Mhe. Mwenyekiti, nataka kumwambia kwamba kutokana na kwamba waziri amesema kuna kifungu kinachomruhusu yule dereva kuendesha ile gari ya kutembeza kupelekwa sehemu husika. Je, kama gari imepata tatizo la kumgonga mtu ambaye anatakiwa kupata *insurance* kwa zile *insurance* za gari zinazotembea yule mtu atapata kifungu gani kitakachomtetea *insurance* wakati ile gari haina *insurance* au hicho kifungu ndio kitasaidia kwamba ndio atakuwa na *insurance* yule mtoto.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Nimesema hivi kwamba gari inapotoka bandarini kwenda katika kituo husika kwa mtu husika kwa hivyo pale inaruhusiwa kulingana na kifungu hichi cha sheria kwa hivyo, yule anaetoa gari bandarini anajua kwamba kwa kipindi kile gari ile haina *insurance* lakini sheria inamruhusu kufika katika *destination* ile ambapo gari inapelekwa, sasa kwa bahari mbaya kama anaichukua ile gari anakwenda huko anakofika wakati gari iliruhusuwa lakini ikatokea ajali hicho ni kitu chengine.

Kwa sababu hapo ni suala la uzembe lakini sio suala la sheria iliyomtoa yeye kutoa gari bandarini kwenda anakokwenda. Kwa hivyo, wanao husika na usalama barabarani watajua utaratibu gani na hatua gani za kumchukulia mtu huyo kwa kumgonga mtoto anayepita barabarani lakini si kwa kutoa gari bandarini kufika kule anakokwenda kwa sababu pale tayari sheria imemruhusu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, katika majibu aliyokuwa kajibu Mhe. Waziri (b) alisema si ruhusa gari kufanya kazi ya kupakia abiria na mizigo je ni nilikuwa nataka kuumuliza tu Mhe. Waziri. Je, ni ruhusa mawaziri siku za *holiday* kutumia magari katika shughuli zao wakati ukizingatia tumepewa pesa wajumbe wote kununua gari zetu hii ni ruhusa au sio ruhusa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri hili swali naona ni swali jengine hili haliko katika swali la msingi. Kwa kwa hivyo unaweza usilijibu, Mhe. Waziri ahasante. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, mbele yetu katika ukumbi wetu hapa tuna wageni ambao kuwa ni wageni wa Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis pamoja na Mhe. Salma Mussa Bilal wa Viti Maalum. Hawa ni viongozi wenyeviti wa UWT ngazi mbali mbali kutoka Kusini Unguja, naomba niwataje wageni wenyewe.

1.	Ndg. Shemsa Abdalla Ali	Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Kusini Unguja.
2.	Ndg. Jina Malik Samala	Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Kusini
3.	Ndg. Riziki Mohamed Abdalla	Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Kati
4.	Ndg. Maryam Pandu Pweleza	Mwenyekiti wa UWT Jimbo la Paje
5.	Ndg. Kidawa Haroun	Mwenyekiti wa UWT Jimbo la Makunduchi
6.	Ndg. Bahati Issa	Mwenyekiti wa UWT Jimbo la Tunguu
7.	Ndg. Nawaje Mussa Vuai	Mwenyekiti wa UWT Jimbo la Uzini
8.	Ndg. Maryam Ussi Khamis	Mwenyekiti wa UWT Jimbo la Chwaka.

Waheshimiwa Wajumbe, wengine ni wageni wa Mhe. Yussuf Hassan Iddi wa Jimbo la Fuoni na Mhe. Nassor Salim Ali Aljazira Jimbo la Kikwajuni. Hawa ni vijana wa timu ya miguu na washindi wa mashindano ya Jimbo Club, ambapo timu yao ya *Jumba Zuri Sports Club* iliilaza timu ya Fuoni Migombani kwa mikwaju ya *penalty* 5 kwa 4. Jumla yao ni 30, lakini wanaongozwa na bi Matina Raphael Kipungani na Sheha wa Shehia ya Fuoni na Ndg. Amina Hassan Ameir Kipungani Diwani wa Wadi ya Fuoni. *(Makofi)*

Kwa ujumla wao wote tunawakaribisha, karibuni katika ukumbi wetu, karibuni sana muone shughuli zetu zinavyoendelea. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

KAULI ZA SERIKALI

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba nichukuwe fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufanikisha majukumu yetu ya kikatiba kwa kipindi cha mwaka 2015/2016 na kukamilisha kazi zetu za ukaguzi kwa wakati muafaka.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa jitihada zako unazochukua katika kuimarisha utawala bora na kupelekea kuimarika kwa nidhamu ya matumizi na rasilimali za umma. Aidha, nitoe shukrani za dhati kwako kwa kupokea Ripoti ya Ukaguzi na Udhibiti wa Hesabu kwa mwaka 2014/2015, kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji katika matumizi ya fedha na rasilimali ya umma.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuwasilisha ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2015/2016, ambapo kwa mwaka huo tumefanikiwa kukamilisha ukaguzi wa mahesabu ya serikali kuu, mashirika ya serikali pamoja na miradi ya maendeleo yaliyokaguliwa kwa kipindi hicho. Lengo la kufanya ukaguzi huo ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na uwajibikaji wenye kuleta tija na ufanisi katika kila rasilimali inayotumika kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua nafasi hii maalum kumshukuru sana Mwenyekiti wa *PAC* pamoja na kamati yake yote kwa mashirikiano yao mazuri sana wanayotupa katika kuendeleza shughuli nzima za sehemu hii.

Mhe. Mwenyekiti, ni matumaini yangu ripoti hii itafanyiwa kazi na kamati inayohusika na kuchunguza na kudhibiti mahesabu ya serikali *PAC*, na kuweza kupata taarifa na uhalisia wa mwenendo mzima wa mapato na matumizi ya fedha na rasilimali za umma kwa mwaka huu.

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali anawajibika kikatiba kukagua hesabu zote za mawizara, taasisi za serikali pamoja na mashirika ya umma na baadae kutoa taarifa ya ukaguzi kwa mahesabu hayo kila mwaka. Kwa mujibu wa kifungu cha katiba 112 Sehemu ya Tatu Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Mdhibiti na Mkaguzi wa Mahesabu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ana wajibika kufanya yafuatayo. Naomba kunukuu.

Kifungu A, kinasema;

a) "Kuhakikisha kwamba fedha zote zinazokusudiwa kutolewa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, matumizi yake yameidhinishwa na iwapo atatosheka kwamba masharti hayo yametekelezwa ipasavyo, basi ataidhinisha fedha hizo zitolewe;

b) Kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo matumizi yake yameidhinishwa yanatokana na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, au fedha ambazo matumizi yake yameidhinishwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi, na ambazo zimetumika kwa ajili ya shughuli zinazohusika na matumizi ya fedha hizo, na kwamba matumizi yamefanywa kwa kufuata idhini iliyotolewa kuhusu matumizi hayo; na

c) Angalau mara moja kwa kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar,

hesabu za mahakama zote za Zanzibar, hesabu za tume au vyombo vyengine vinavyohusika na Baraza la Wawakilishi".

Mhe. Mwenyekiti, tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti ya mwaka 2014/2015. Mhe. Mwenyekiti, katika ukaguzi uliyofanyika imebainika kwamba serikali imetekeleza mapendekezo na ushauri uliotolewa katika Ripoti na Mdhibiti wa Mahesabu ya Serikali kwa mwaka 2014/2015. Imebainika kwamba mafanikio makubwa yamepatikana katika ufungaji na uwasilishaji wa hesabu za mwisho wa mwaka na kupelekea kuimarika kwa uwajibikaji katika usimamizi na matumizi ya rasilimali za umma katika mawizara, mashirika na taasisi za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, mafanikio haya yanatokana na jitihada zilizochukuliwa na serikali katika kufuatilia na kusimamia ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali, zinazowasilishwa kwako kila mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, upeo na madhumuni ya ripoti ya mwaka 2015/2016. Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2015/2016 Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu imefanya ukaguzi wa mahesabu na kutoa ripoti ya ukaguzi kwa mawizara, taasisi na mashirika ya serikali ya Zanzibar pamoja na baadhi ya miradi ya maendeleo yaliyowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. Ripoti hizo zimekusanya taarifa mbali mbali za mapato na matumizi ya mawizara, mashirika na miradi ya maendeleo pamoja na taarifa za mapato na matumizi ya Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, ukaguzi wa mahesabu hayo ulifanywa kwa mujibu wa viwango vya kitaifa na kimataifa vya ukaguzi, ambapo sheria, kanuni, miongozo na taratibu za uhasibu za ukaguzi zilizingatiwa. Aidha, ukaguzi uliangalia viashiria vya maeneo hatarishi katika taasisi zilizokaguliwa kwa lengo la kupata uelewa na mazingira ya taasisi hizo, ukiwemo mfumo wa udhibiti wa ndani pamoja na utendaji wa taasisi hizo.

Mhe. Mwenyekiti, mambo yaliyobainika katika ukaguzi wa mwaka 2015/2016. Katika mwaka huu hali ya uwekaji wa kumbukumbu za mahesabu na taasisi mbali mbali za serikali umeimarika, na kufanikiwa kukamilika kwa ufungaji wa mahesabu ya mwisho wa mwaka kwa wakati na kuwasilishwa kwa ajili ya kukaguliwa kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, kuimarika kwa uwekaji wa kumbukumbu na mahesabu ya serikali na ufungaji wa hesabu, kumepelekea kuimarika kwa uwazi na uwajibikaji katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha na rasilimali za umma, ambapo kumekuwa na ongezeko kubwa la mapato mwaka hadi mwaka na kupelekea kuimarika kwa hali ya uchumi na kufanikiwa kutekeleza malengo yake yaliyopangwa na serikali.

Mhe. Mwenyekiti, taarifa ya mapato na matumizi kwa mwaka 2015/2016. Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi cha mwaka 2015/2016 mapato yaliyokadiriwa kukusanywa ni jumla ya shilingi bilioni 330,830.4. Makadirio haya yalitarajiwa kutoka katika vyanzio mbali mbali, ikiwemo mikopo, misaada ya kibajeti na washirika wa maendeleo, ambapo jumla ya shilingi milioni 429.5 bilioni zilitarajiwa kutoka ndani na jumla ya shilingi bilioni 400.9 zilitarajiwa kutokana na

misaada ya kimaendeleo kutokana na washirika mbali mbali wa kimaendeleo, pamoja na mikopo ya ndani yenye jumla ya shilingi 20.857 bilioni.

Mhe. Mwenyekiti, taarifa ya matumizi. Kwa upande wa matumizi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitarajiwa kutumia jumla ya shilingi 830.4 bilioni, ambapo shilingi 883.3 bilioni ni kwa kazi za kawaida na shilingi bilioni 347.1 ni kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, mapato na matumizi kwa kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Mhe. Mwenyekiti, ukaguzi umebaini kwamba hadi kufikia tarehe 30 Juni 2016, mapato ya ndani yaliyokusanywa ni jumla shilingi bilioni 422.381 sawa na asilimia 98.3 ya makadirio, ikiwa ni upungufu wa asilimia 7.119 sawa na asilimia 1.7 ya upungufu. Aidha, mapato yanatokana na misaada ya kibajeti yalifikia jumla ya shilingi bilioni 7.674. Ukaguzi umebaini kwamba makusanyo ya ndani yameongezeka kwa mwaka 2015/2016 na kufanya jumla ya shilingi 422.381 bilioni, ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2014/2015, ambapo makusanyo halisi yalikuwa ni shilingi 354.4 bilioni, ongezeko hilo ni shilingi 67.981 bilioni, ambalo ni sawa na 19.2.

Mhe. Mwenyekiti, taarifa ya matumizi ya kazi za kawaida. Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016 serikali ilikadiria kutumia shilingi 431,714,021,000 bilioni, kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida katika Mfuko wa Hazina. Serikali ambapo jumla ya shilingi bilioni 402,446,410,000 zimetumika kwa kazi mbali mbali za kawaida na asilimia 93.2 ya makadirio ikiwa na upungufu wa shilingi bilioni 29,207,611,000 sawa na asilimia 6.8 ya makadirio.

Mhe. Mwenyekiti, taarifa ya matumizi ya kazi za maendeleo. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016 serikali ilikadiria kutumia kiasi cha shilingi bilioni 51,880,000,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo katika Mfuko wa Hazina ya Serikali, ambapo jumla ya shilingi bilioni 37,823,042,000 zimetumika kwa kazi mbali mbali za maendeleo, sawa na asilimia 73 ya makadirio, ikiwa ni upungufu wa shilingi bilioni 14,056,958,000, sawa na asilimia 27 ya makadirio.

Mhe. Mwenyekiti, taarifa ya jumla ya matumizi ya serikali. Matumizi ya serikali kwa jumla kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ilikuwa ni kama ifuatavyo. Matumizi ya kawaida yameongezeka kutoka shilingi bilioni 348,336,223,000 kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Hadi kufikia shilingi bilioni 402,446,410,000 kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kukiwa na ongezeko la bilioni 54,080,117,000 sawa na asilimia 15.5 ya ongezeko.

Mhe. Mwenyekiti, kazi za maendelo. Matumizi ya maendeleo yamepungua kutoka shilingi bilioni 47,764,283,000 kwa mwaka wa fedha 2014/2015, hadi kufikia bilioni 37,823,042,000 kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kwa kiasi cha upungufu wa bilioni 10,941,241,000, ikiwa ni sawa na asilimia 22.4.

Aidha, ukaguzi umebaini kwamba kwa ujumla matumizi ya serikali yameongezeka kutoka shilingi bilioni 397,130,676,000 kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Hadi kufikia shilingi bilioni 440,269,452,000 kwa mwaka wa fedha 2015/2016, kwa kiasi cha ongezeko la shilingi bilioni 43,138,776,000 sawa na asilimia 10.9.

Mhe. Mwenyekiti, malengo ya baadae. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali itaendelea na juhudi zake za kuimarisha utawala bora, kwa kufanya kazi ya ukaguzi wenye tija na ufanisi na kuhakikisha kwamba rasilimali za umma zinatumika ipasavyo kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji. Ofisi imekamilisha utekelezaji wa mpango mkakati wa mwaka 2014/2017 ambapo utekelezaji wa mpango mkakati huo ulileta tija na mafanikio makubwa katika ofisi kwa kuimarika kwa utendaji wa kazi za ukaguzi, ikiwemo upatikanaji wa vitendea kazi pamoja na wafanyakazi kupelekea kuimarika na huduma zinazotolewa.

Aidha, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali, imetayarisha mpango mkakati mwengine kwa miaka mitatu, kuanzia mwaka 2017/2020 ambapo mpango mkakati huo umejikita katika kuimarisha utendaji kazi za ukaguzi ikiwemo upatikanaji wa vitendea kazi, pamoja na wafanyakazi wenye taaluma katika kada mbali mbali zinazosaidia kuimarisha kazi za ukaguzi. Ofisi itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kikatiba kwa kuzingatia Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, sheria na taratibu zilizopo kitaifa na kimataifa.

Shukrani. Mhe. Mwenyekiti, napenda nichukuwe nafasi hii kutoa shukrani kwa wote watakaochangia kwa njia moja au nyengine. Kuanzia kazi ya ukaguzi, ufuatiliaji wa maeneo mbali mbali yaliyokaguliwa hadi kukamilika kwa ripoti hii ya ukaguzi ambayo naiwasilisha leo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukuwe fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa jitihada zake anazochukua kuimarisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu, katika kusimamia uwajibikaji wa matumizi ya rasilimali za umma kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar. *(Makofi)*

Aidha, natoa shukrani kwa viongozi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa jitihada zao mbali mbali wanazochukua katika kusimamia nidhamu na uwajibikaji wa matumizi na rasilimali za umma kwa kila sekta.

Vile vile, napenda kuwapongeza na kuwashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali, kwa juhudi zao wanazochukua hadi kufanikisha kukamilika kwa ripoti hii kwa wakati. Halikadhalika nawashukuru viongozi na watendaji wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na watendaji wa taasisi mbali mbali wa serikali kwa mashirikiano mazuri wanayotupa wakati wakati wa kutekeleza kazi zetu za kiukaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuishukuru kwa dhati kabisa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali *(PAC)* na Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, pamoja na wale wote waliochangia kwa njia moja ama nyengine katika kuleta maendeleo katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati ya Baraza la Wawakilishi ni muhimu sana katika kuimarisha uwajibikaji na kuleta ufanisi katika kufikia malengo ya serikali iliyojipangia. Kamati hii inatoa mchango mkubwa katika kujenga na kusimamia misingi ya utawala bora na uwajibikaji kwa matumizi ya rasilimali za umma.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na umuhimu mkubwa kamati ya Baraza la Wawakilishi ya ofisi imekuwa ikishirikiana na kamati hizo kwa kufuatilia utekelezaji wa bajeti za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, pamoja na kuhakikisha kwamba taasisi za serikali zinatekeleza malengo waliyojipangia kama ilivyoainishwa katika bajeti zilizoainishwa na Baraza la Wawakilishi.

Aidha, Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali *PAC,* inatoa mchango mkubwa katika kusimamia uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma. Kamati hii imekuwa ikishirikiana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali katika kufuatilia ripoti zake na kutoa ushauri na mapendekezo mbali mbali kwa serikali, kwa lengo la kuimarisha ufanisi, uwazi na uwajibikaji kwa matumizi ya rasilimali hizo kwa maendeleo ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, tunatoa shukrani za dhati kwa wenyeviti na wajumbe wa kamati zote za Baraza la Wawakilishi, kwa jitihada zao wanazochukua kusimamia uwajibikaji katika kuleta na kutekeleza majukumu yao kwa sekta mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, shukrani za pekee ziwaendee wenyeviti na wajumbe wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali pamoja na Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa jitihada mbali mbali inazochukua katika kutoa maoni yao na ushauri wa ofisi pamoja na serikali, ambapo ushauri wao na maoni ya michango yao imesaidia kuimarisha uwajibikaji na nidhamu na matumizi ya rasilimali za umma.

Changamoto. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mafanikio ya kiutendaji yaliyopatikana ofisi inakabiliwa na changamoto mbali mbali katika utekelezaji wa kazi za ukaguzi, ikiwemo mabadiliko ya mara kwa mara ya teknolojia na mifumo ya wahasibu wakaguzi inayotokea duniani, ambapo yanaathiri utendaji wa kazi kwa vile yanahitaji rasilimali nyingi ili kukabiliana na changamoto hizo.

Kwa kupambana na changamoto hizo ofisi imejipanga kuimarisha utendaji wa kazi, kwa kuwapatia wafanyakazi wake vitendea kazi vinavyokidhi mahitaji ya mabadiliko ya kiteknolojia, pamoja na kuwapatia mafunzo mbali mbali ya ukaguzi, ikiwemo maadili ya ukaguzi, uaminifu, uadilifu na uwajibikaji katika kazi. Ni imani yangu kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea na jitihada zake za kuimarisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali, kwani ofisi hii ndio jicho la serikali katika kuimarisha uwazi na uwajibikaji kwa maendeleo ya wananchi wa Zanzibar na kuimarisha dhana nzima ya utawala bora.

Hitimisho. Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine tena natoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi, kwa mikakati uliyoichukua ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na uwajibikaji kwa lengo la kuimarisha utawala bora. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu itaendelea kuunga mkono juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, katika kusimamia uwajibikaji na uwazi kwa matumizi ya rasilimali za umma, ili kufikia utawala bora wenye kuheshimu misingi ya sheria na taratibu ziliopo. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana. Sasa nitamwita Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (*PAC*), ili aweze kuwasilisha hotuba yake ya maoni.

Mhe. Shaib Said Ali (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika): Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* naomba sasa kuwasilisha hotuba ya maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika juu ya uwasilishaji wa ripoti na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar, kwa kipindi cha mwaka 2015/2016.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Bwana wa viumbe vyote kwa kutujaalia uhai, afya njema na taufiki ya kuweza kukutana hapa leo kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu muhimu ya kikatiba ya kuisimamia serikali na kuwawakilisha wananchi wa Zanzibar katika kufanya maamuzi muhimu ya kitaifa.

Aidha, naomba nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kwa ajili ya kuzungumza machache na ya muhimu, yanayohusu uwasilishwaji wa ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2015/2016 kama ambavyo Kanuni ya 43(1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2016 inavyoelezea.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii pia kumshukuru Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kuweza kuwasilisha hapa Barazani ripoti hizi ambazo ndizo nyenzo kuu za kazi ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*). *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, napenda kutoa pongezi na shukurani za dhati kwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati hii ya *PAC* kwa mashirikiano yao makubwa wanayoendelea kuyaonesha katika utekelezaji wa kazi za Kamati hii. Ni ukweli usiopingika kwamba mashirikiano na moyo wa kujitolea walionao ndio chachu inayoifanya Kamati hii kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wao, naomba niwatambue kwa majina Wajumbe na Makatibu hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Mwenyekiti.
2. Mhe. Shaib Said Ali - Makamu Mwenyekiti.
3. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Mjumbe
4. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Mjumbe
5. Mhe. Salma Mussa Bilali - Mjumbe
6. Ndg. Nasra Awadh Salmin - Katibu
7. Ndg. Haji Khatib Haji - Katibu

Mhe. Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuwapongeza kwa dhati viongozi na watendaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa kazi nzuri wanazoendelea kuzifanya za kufuatilia mapato na matumizi ya fedha za umma zinazotumika kwa shughuli mbali mbali za uendeshaji wa serikali, licha ya changamoto mbali mbali zinazowakabili. Ofisi hii imefanya kazi kubwa na nzito ya kufanya ukaguzi katika mawizara, mashirika na taasisi mbali mbali za serikali, na kuandaa ripoti hizi kama ambavyo kifungu cha 112 cha katiba yetu kinavyoeleza.

Mhe. Mwenyekiti, kama inavyoonekana kuwa ripoti hizi zimesheheni mambo mengi, makubwa na yaliyohusisha mapato na matumizi ya fedha nyingi za serikali, na hivyo kuhitaji kufanyiwa kazi kwa kina na kwa umakini mkubwa, na kwa kuwa ripoti nyengine kama hizi zinatarajiwa kuwasilishwa hapa Barazani katika mwaka 2019/2020. Hivyo basi, Kamati ya *PAC* inaiomba ofisi yako ifikirie kuiongezea muda zaidi wa kufanya kazi kamati hii, ili iweze kufanya kazi kwa weledi na ufanisi mkubwa bila ya kuripua na kuikamilisha kazi hii kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, nakuomba nirudie kifungu hiki, kama inavyoonekana kuwa ripoti hizi zimesheheni mambo mengi makubwa na yanayohusu mapato na matumizi ya fedha nyingi za Serikali na hivyo kuhitaji kufanyiwa kazi kwa kina na kwa umakini mkubwa. Kwa kuwa ripoti hizi nyengine kama hizi zinazotarajiwa kuwasilishwa hapa Barazani katika mwaka 2019/2020 hivyo basi Kamati ya *PAC* inaiomba ofisi yako ifikirie kuiongezea muda zaidi wa kufanyakazi kamati hii ili iweze kufanya kazi kwa uweledi na ufanisi mkubwa bila ya kuripua na kuikamilisha kazi hii kwa wakati unaotakiwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Jadweli la Kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2016, linaeleza kuwa, Kamati ya *PAC* pamoja na mambo mengine ndio yenye jukumu la kuchunguza na kutoa taarifa juu ya hesabu ya mwaka ya matumizi ya fedha za serikali na mashirika yake na hesabu nyengine zote zitakazowasilishwa mbele ya Baraza kupitia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Hivyo, naomba nitamke kuwa Kamati ya *PAC* inaipokea ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Mwenyekiti, kamati hii inaahidi kuwa itazifanyia kazi ipasavyo ripoti hizo na hatimae kuwasilisha ripoti yake kwa kina hapa Barazani katika muda muafaka, kama Kanuni za Baraza hili zinavyoelekeza.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuzipokea ripoti hizo kamati ya *PAC* imebaini kuwa baadhi ya Mashirika bado ripoti zao za ukaguzi hazijawazilishwa Barazani tokea kamati hii ilivyoanza shughuli zake mwaka 2016, ingawa Mashirika haya yanaendelea kutekeleza shughuli zake. *(Makofi)*

Mashirika yenyewe ni kama yafuatayo:-

1. Shirika la Bima Zanzibar (*ZIC*)
2. Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*)

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hilo yapo baadhi ya mashirika na taasisi za umma ambazo katika ripoti ya mwaka wa fedha 2014/2015 na 2015/2016 hazijawasilishwa taarifa zake za ukaguzi jambo ambalo ni kwenda kinyume na matakwa ya sheria inayohusiana na masuala ya fedha. Mashirika na taasisi zenyewe ni:-

1. Chuo cha Uongozi wa Fedha (*ZIFA*)
2. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (*ZAA*)

3. Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*).

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, yapo baadhi ya mashirika ambayo hayawasilishi taarifa zake zao za ukaguzi katika ripoti ya mwaka 2015/2016. Mashirika yenyewe ni haya yafuatayo:-

1. Shirika la Umeme Zanzibar (*ZECO*)
2. Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*)
3. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (*ZSSF*).

Mhe. Mwenyekiti, kwa msingi huo, Kamati ya *PAC* hairidhishwi na hali hiyo, hivyo tunaisisitiza Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kuhakikisha kuwa wale wote wanaoidhinishiwa fedha za matumizi wanakaguliwa kila mwaka na taarifa zao zinawasilishwa mbele ya Baraza la Wawakilishi kwa hatua zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tunasisitiza hili kwa kuwa siku chache zijazo tunatarajia ofisi hii kuajiri wafanyakazi wapya, jambo ambalo ilikuwa ni kilio kikubwa cha ofisi hii kutokana na kukosekana kwa muda mrefu kwa Bodi ya Utumishi ya Ofisi ya Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali. Bodi ambayo hivi karibuni Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alimteua Mwenyekiti wa Bodi hiyo na kupelekea Mhe. Waziri husika kuteua Wajumbe wawili wa Bodi hiyo kama sheria inayohusiana na Ofisi ya Mdhibiti inavyoelekezea.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sasa taratibu zote zinazopaswa kufanyiwa wafanyakazi wanaotarajiwa kuajiriwa na ofisi hii kwa mujibu wa sheria inayohusiana na masuala ya utumishi zimekamilika. Hivyo basi, Kamati ya *PAC* inaiomba Bodi ya Utumishi ya Ofisi ya Mdhibiti kuendelea na hatua zilizosalia ili kukamilisha zoezi hilo haraka iwezekanavyo na kuwapatia ajira vijana hao kwa kuwa ni muda mrefu sasa wanasubiria ajira hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia naomba kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, kwa kunisikiliza kwa makini na kwa utulivu mkubwa wakati nilipokuwa nikiwasilisha hotuba yangu hii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Ahsante sana.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, Mhe. Makamu Mwenyekiti. Waheshimiwa Wajumbe, naomba nikumbushe kidogo katika utaratibu wetu wa leo kuhusu Kauli ya Serikali, kwa mujibu wa kanuni zetu za Baraza la Wawakilishi Kanuni ya 43 kifungu namba 3 naomba nikisome ifuatavyo.

Kanuni ya 43(3) inasema hivi:

> “Hakutokuwepo na majadiliano yoyote kuhusu kauli yoyote iliyoletwa na kwa mujibu wa kanuni hii, lakini Wajumbe wanaweza kwa idhini ya Spika kumuuliza maswali Mhe. Waziri aliyetoa kauli hiyo kwa madhumuni ya kuelewesha zaidi juu ya maelezo ya kauli hiyo”.

Hivi ndivyo inavyosema kanuni yetu na tutaifuata. Kwa sasa nina watu watatu ambao nitawaruhusu hao kumuuliza Mhe. Waziri, ili aweze kutoa majibu. Ahsanteni sana. Mtu wa kwanza nitamruhusu Mhe. Suleiman Sarhan Said.

Mhe. Suleiman Sarhan Said: Nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti kwa kupata fursa hii ya kuuliza maswali machache. Katika ripoti hii niliyoisikia niliona kuna kitu kimoja ambacho ni ucheleweshaji wa ripoti kwa wakati kutokana na hali halisi inakuwa ripoti inapofika inakuwa kama haileti manufaa yalikusudiwa hasa. Lakini swali la pili nimeona katika ripoti hii ni kwamba hati zote zimeridhishwa wakati tumeona humu tukiweka mabuti na mambo mengine ambayo ya mashirika na matatizo kama kamati inavyozungumza. Lakini bado mashirika yote yamepata hati inayoridhisha kuna hati za aina nne iliyotumika zaidi na iliyofanikiwa zaidi ni kwamba wote wamepata hati.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, uulize swali usichangie hotuba.

Mhe. Suleiman Sarhan Said: Ndiyo maswali yenyewe Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu nilitaka niulize na *question mark*, maana yake namuuliza najua kwamba kuchelewa kwa ripoti ni sababu gani zinazosababisha kuchelewa kwa ripoti, ndiyo swali ni hilo Mhe. Mwenyekiti isipokuwa ni vingine tu.

Vile vile, ni sababu gani zilizofanya kwamba ripoti zote kuwa na hati inayoridhisha wakati kuna mambo mengi ambayo pamoja kamati ya imeelekezwa kwamba kuna kasoro zilizojitokeza.

Mhe. Mwenyekiti, sababu gani ambazo zilizoshindwa kujipanga kwa wataalamu na kupata vifaa vya kisasa kwa kujua umuhimu wa suala hili.

Lakini swali la mwisho, serikali imejipanga vipi kuhusu ajira za vijana. Ahsante kwa kunipa nafasi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, sasa naomba nimwite Mhe. Mohammed Said Mohammed, aweze kuuliza swali.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nikushuru sana kwa kuniona, kwanza nichukue fursa hii sana kuwapongeza kamati kwa kusema ukweli lakini kwa kujua majukumu ya wananchi na *concern* yangu ya jana wameweza kuijua vizuri sana kuhusu taasisi na serikali binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, tumepata ripoti ya 2015/2016 nilikuwa nataka kuiuliza serikali tu kwa kuwa 2015/2016 imeshapitwa na wakati muda mwingi sana. Je, serikali ina mpango gani hasa wa kufanya ripoti hizi kuwa mwaka mmoja tu nyuma, ili kuweza kuweka uwiano sawa na kuweza kuwa na uwajibikaji katika serikali yetu (*makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, la pili mwaka 2015/ 2016 Katibu Mkuu Kiongozi aliinuka kwenye vyombo vya habari kutangaza kuwa kuna wafanyakazi hewa wengi sana, lakini cha kushangaza sana katika ripoti hii hati zote zilizopatikana ni hati safi au za kuridhisha na nimejaribu kusoma vipi

hati safi zinakuvyokuwa, vipi hati chafu zinavyokuwa lakini na kutokuridhisha, sasa sioni mantiki hiyo ningeomba kauli ya serikali juu ya jambo hilo.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, muuliza swali jengine ni Mhe. Machano Othman Said.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na niungane na wenzangu ambao wameuliza maswali na mimi niulize swali moja. Katika ukurasa wa 88 wa ripoti hii ya *CAG*, matokeo ya uchunguzi yamebainisha kwamba *ZMUX* wametumia 73,536,000 ambazo hazionekani katika vitabu vya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo iliyokuwa, lakini hatimae katika majumuisho wamepewa hati ambayo inaridhisha, sasa sisi tunataka kujua hizi vigezo jamani vinakuwaje na ili upate hati chafu inakuwa vipi, maana yake naona milioni 73 hazikutumika vizuri lakini bado hati inaridhisha. Nataka kujua hilo.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, namuuliza swali wetu wa mwisho atakuwa ni Mhe. Simai Mohammed Said, basi Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini subiri atakapomaliza Mhe. Simai Mohammed Said.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii kuuliza maswali mawili madogo. Swali langu la kwanza linafanana kabisa na Wajumbe waliotangulia, ni hofu ambayo tunakuwa tunaipata kwamba tunaangalia hapa ripoti ya 2015/2016 wakati leo tupo mwaka 2018.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka kufahamu kabla ya kuichangia ripoti hii. Je, Mhe. Waziri anatuhakikishia vipi kwamba zile taasisi ndani ya serikali ambazo katika mwaka ule ama kwa njia moja au nyingine hasa katika sekta binafsi walikuwa wana madeni ambayo yaliingizwa, kwa mfano ukichukua kuanzia ukurasa wa 37 kuhusu mabango, mapato, leseni za biashara, kodi ya pango, mambo haya kawaida wanakuwa wanaendelea kudaiwa. Sasa je, Mhe. Waziri tunapokuja kuchangia sisi ripoti hii wakati utakapofika atahakikisha vipi kwamba hizi taasisi kwa njia moja au nyengine zilizokuwa zinadaiwa tayari wao wameshajirekebisha na hatumtii kwa sababu kumtaja mtu na jina lake hapa ni sehemu kubwa sana, lakini kama kule deni lake tayari deni lake ameshalipa tunakuja kumjadili hapa 2015/2016 itakuwa hatumtendei haki.

Sasa namuomba Mhe. Waziri atuambie atahakikisha vipi kwamba hao ambao wametajwa humu ndani watakuwa wao pia anawalinda. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante. Sasa naomba nimwite Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini naye aweze kuuliza swali.

Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, nakushuru sana kunipa wasaa wa kuuliza swali moja tu, kwanza tumpongeze sana Mhe. Waziri kwa ripoti yake pamoja na Mwenyekiti wa *P.A.C* kwa niaba ya kamati.

Lakini kwa kweli, kazi nzuri iliyofanywa na ofisi ya *CAG* nayo inahitaji kupongezwa. Swali je, Mhe. Mwenyekiti tumezowea kwa wenzetu tunaona katika misingi ya utawala bora vitu kama hivi vinawekwa wazi ndiyo *transparency* hiyo, na hiyo ndiyo nguzo moja wapo ya utawala bora.

Je, watamruhusu *CAG* kufanya *Press Conference* na yeye kutoa *finding* zake kama alizozileta Barazani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante. Waheshimiwa Wajumbe, naomba tutambue, katika ukumbi huu tuna Bodi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ipo hapa mbele yetu katika sehemu ya juu kule, ambayo ilikuwa ikiongozwa na Mhe. Balozi Mohammed Ramia. (*Makofi*).

Mhe. Jaku Hashim Ayoub, atakuwa muulizaji wa swali la mwisho.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze sana kamati ya *PAC* kwa umakini wake, lakini nitakuwa sijawafanyia haki makatibu wa kamati hii kwa umakini wa hali ya juu. Niwapongeze sana makatibu wa kamati.

Mhe. Mwenyekiti, ninachozungumza sasa hivi ni kiswahili, nilikuwa nataka kufahamishwa na kuelimishwa kanuni za serikali, lugha ya Baraza ni kiswahili kwa mujibu wa Katiba, miongoni mwa sifa za kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa kifungu cha 68 ni kusema lugha ya Kiswahili.

Je, kwa nini hesabu za mwisho za mwaka za mashirika na taasisi za umma za mdhibiti zinaandikwa kwa lugha ya Kiingereza swali langu lipo hapo na lugha tunayotumia ni kiswahili hilo la kwanza.

Pili, kamati ilitaja hapa suala la *ZSTC* karibu Baraza la tisa kwa nini hesabu zake hazipatikani, tuelimishwe tuelezwe. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, tumemaliza Waheshimiwa Wajumbe kuuliza maswali. Sasa nimwite Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia leo kufika mwezi ishirini na tisa Ramadhani, lakini pia nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii tena kutoa baadhi tu ya jawabu. Lakini kama ulivyotoa mwanzo kanuni ilivyoeleza ni sahihi kabisa kwamba hakuna maoni, hakuna kuhoji ni kuuliza maswali tu, sasa maswali waliyoulizwa mengi yamefanana na nitayajibu kwa pamoja lakini zaidi ya hivyo majibu mengine na taarifa nyingine za ndani zitapatikana wakani *PAC* ikishafanya kazi zake.

Kwa nini ripoti hii imechelewa, imekuja mwaka 2015/2016, nataka nikumbushe Waheshimiwa Wajumbe wakumbuke historia huko nyuma tulikuwa tunakaa miaka mitatu minne hatupokei ripoti kama hivi, na lazima tumpongeze sana Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa kazi anazozifanya angalau tuko nyuma mwaka mmoja au mmoja na nusu, kazi nzuri sana amefanya huko nyuma tulikuwa tunakaa miaka miwili, mitatu hatujapokea ripoti yotote. Leo angalau tumefika 2015/2016 na hivi ninavyosema kwamba ya mwaka 2016/2017 nayo iko katika hatua za mwisho na tunatarajia kuiwasilisha kwa mujibu wa utaratibu wa kisheria ya kikatiba Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, swali la pili kwa nini suala la ajira halijafanyika mpaka leo limechelewa sana, suala la ajira limechelewa kwa sababu kulikuwa na matatizo. Ofisi hii ilikuwa haina Bodi amabayo inaweza ku-*oparate* na suala la ajira la ofisi hii lazima lisimamiwe na bodi yenyewe sasa hivi Bodi imekamilika Mwenyekiti tayari na kuna wajumbe tumeshawateua wako tayari kwenye Bodi hii na tunatarajia tukijaaliwa *inshallah* katika kipindi kifupi sana suala la ajira hili litapata ufumbuzi na wale wote ambao walishughulikia kufanya ajira hii basi watapata majibu yao kwa mujibu wa utaratibu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, swali la mwisho kwa nini kuna hati chafu na hati safi na ripoti zinasema hivyo. Mhe. Mwenyekiti, unajua unapopata hati chafu kuna ushahidi wa kutosha kwamba kuna upotevu mkubwa wa pesa. Lakini hati zinaridhisha, lakini siyo kwamba zile taarifa hazikuonekana siyo kama hazipo pengine hazikuonekana siku alipokwenda tu mkaguzi kukagua pale, lakini ripoti zake au risiti zake pengine zipo au vielelezo vyake vipo.

Kwa hivyo hatuwezi kumuandikia hati chafu mtu kama yule lazima tutasema kwamba taratibu zetu, ukitizama utaratibu wa kuweka mahesabu na namna yalivyokwenda na hesabu zilivyomalizika zilivyofungwa anaridhika Mkaguzi kwamba hesabu zimekwenda vizuri hakuna ushahidi kwamba kuna upotevu wa pesa. Kwa hiyo, huwezi kupata hati chafu kama ripoti yako inaridhisha, sasa nataka wafahamu hivyo tu kwamba utaratibu huu ni wa kawaida wa kuandika ripoti pale ukishafika kama hukugundua jambo lolote la upotevu mkubwa wa fedha basi umepata.

Vile vile, kuhusu swali lile la Mhe. Mohammed Said Mohammed alilozungumza suala lile la taarifa ile ya wafanyakazi hewa ile ni kazi maalum aliyokuwa amepewa na Mheshimiwa aliyemteua alimpa kazi *CAG* kwenda kufanya kazi hiyo. Sasa ile ni kazi maalum ambayo imepelekwa kunako husika na *Chief Secretary* ameshaitolea ufafanuzi sina haja ya kutoa ufafanuzi huo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ufupi nayasema hayo na haya masuala la kilugha na mambo mengine mambo ya kitaalamu kidogo kwa hivyo naomba tupewe muda kidogo, ili Kamati ya *PAC* itakapokuja tulitolee ufafanuzi pamoja na hayo mengine yaliyobakia. Nashukuru sana ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri utoe hoja ili tuweze kuwahoji Wajumbe kuipokea.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti naomba kutoa hoja ya taarifa hii niliyoiwasilisha.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa naomba niwahoji Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe, kama ilivyotoka taarifa ya katibu kwamba shughuli za leo zimemalizika na mimi niwashukuru sana kwa kuweza kuipitisha taarifa hii Kauli ya Serikali na kuweza kuuliza maswali na hadi hapa leo naomba niakhirishe kikao hiki hadi siku ya tarehe 20/06/2018. Baada ya hayo niwashukuru sana.

(Saa 4:40 Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe
20/06/2018 saa 3:00 asubuhi)